TANGAZO LA SERIKALI NA. 73 la tarehe 2/2/2024

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA KIFUNDA YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Kifunda ya Mwaka 2024.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpango wa jumla na kina wa eneo

3. Mpango wa Jumla na kina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo.

JEDWALI

*(Limeandaliwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:-

"Mpaka unaanzia kwenye barabara ya Itete hospitali katika alama ya mpaka namba A yenye majira-nukta 596501MS, 8973103KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Mashariki katika uelekeo wa KZ $84^0$ 29' 08.89 MS kwa umbali wa kilomita 0.62 hadi kwenye alama ya mpaka namba B yenye majira-nukta 597115MS, 8973162KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea KusiniMashariki mwa Mto Lufilyo katika uelekeo wa KS $86^0$ 54'

08.31MS kwa umbali wa kilomita 0.95 hadi kwenye alama ya mpaka namba C yenye majira-nukta 598065MS, 8973111KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Mashariki katika uelekeo wa KZ $81^0$ 27' 19.56 MS kwa umbali wa kilomita 0.68 hadi kwenye alama ya mpaka ya namba D yenye majira-nukta 598746MS, 8973213KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Mashariki katika uelekeo wa KS 30 02' 22.69MS kwa umbali wa kilomita 1.16 hadi kwenye alama ya mpaka namba E yenye majira-nukta 599327MS, 8972209KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea katika uelekeo Kusini-Magharibi katika uelekeo wa KS $19^0$ 27' 57.12MS kwa umbali wa kilometa 0.78 hadi kwenye alama ya mpaka namba F yenye majira-nukta 599301MS, 8972136 KZ;baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Mashariki katika uelekeo wa KZ $89^0$ 59' 20.41MS kwa umbali wa kilomita 2.38 hadi kwenye alama ya mpaka namba G yenye majira-nukta 596915MS, 8972135KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Magharibi katika uelekeo wa KZ$0^0$ 43'14.39 MG kwa umbali wa kilomita 0.25 hadi kwenye alama ya mpaka namba H yenye majira-nukta 596912MS, 8972388KZ;baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Magharibi katika uelekeo wa KZ $37^0$ 56' 51.70 MG kwa umbali wa kilomita 0.62 hadi kwenye alama ya mpaka namba I yenye majira-nukta 596532MS, 8972876KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Magharibi katika uelekeo wa KZ $07^0$ 34' 34.106MG kwa umbali wa kilomita 0.23 hadi kwenye alama ya mpaka namba A yenye majira-nukta 596501MS, 8973103KZ unapoanzia."

Dodoma,
29 Disemba, 2023

JERRY WILLIAM SILAA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*